Asili na Chimbuko la Wazungumzaji wa Kimakunduchi: Hoja za Kihistoria

Mussa M. Hans

Ikisiri

Wakati tukiwa tunasherehekea mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali, hatuna budi kujiuliza katika mijadala yetu ni kwa kiwango gani tumezishirikisha lahaja za Kiswahili katika kubaini mambo mbalimbali ikiwemo historia ya lugha hii. Tukumbuke kwamba wakati wa uteuzi wa lahaja ya Kiunguja kuwa msingi wa usanifishaji wa Kiswahili, ilishauriwa kwamba lahaja nyinginezo za Kiswahili zishirikishwe ipasavyo katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kwa muda mrefu sasa maendeleo ya lugha ya Kiswahili yamekuwa yakijadiliwa bila ya kuzishirikisha lahaja za lugha hii. Matokeo yake ni kwamba kuna hazina kubwa iliyomo katika lahaja hizi ambayo haijatumiwa ipasavyo katika mchakato wa kukuza lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa maeneo yenye mjadala mkali na ambayo lahaja zikishirikishwa vema zinaweza kuwa na mchango mkubwa ni katika historia ya lugha ya Kiswahili, hususani mjadala kuhusu asili na chimbuko la lugha hii. Kwani wataalamu mbalimbali wamekuwa wakihitilafiana kuhusu mahali hasa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili walipotokea. Lengo la makala haya basi ni kujadili kuhusu chimbuko la wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi visiwani Zanzibar.

1.0 Utangulizi

Makala haya ni sehemu ya matokeo ya utafiti uliofanywa na mwandishi huko Zanzibar kwa lengo la kuchunguza mchango wa lahaja za Zanzibar katika kukuza na kuendeleza Kiswahili sanifu. Lengo kuu la makala haya ni kujadili kuhusu chimbuko la wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi. Makala pia yatajadili kwa muhtasari asili ya Kihadimu na Kimakunduchi. Istilahi ya Kihadimu imejadiliwa kwa kuzingatia hoja kwamba kwa muda mrefu waandishi wengi waliokuwa wakijadili kuhusu lahaja za Kiswahili, jina la Kihadimu ndilo lililokuwa likitumika badala ya Kimakunduchi. Kwa kiasi kikubwa data za utafiti wa makala haya zilipatikana kwa kutumia njia ya majadiliano na wazungumzaji wazawa wa Kimakunduchi katika majopo. Ili kuweza kulifikia lengo hili, makala yamegawanywa katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza inaelezea usuli wa lahaja ya Kimakunduchi, sehemu ya pili inajadili kuhusu asili ya majina ya Kihadimu na Kimakunduchi, sehemu ya tatu kwa upande wake inahusu mjadala kuhusu chimbuko la wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na sehemu ya nne ni hitimisho.

2.0 Usuli wa Lahaja ya Kimakunduchi

Kimakunduchi ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili zilizoko katika kisiwa cha Zanzibar. Lahaja hii inazungumzwa katika maeneo mbalimbali yaliyomo katika wilaya ya Kusini Unguja. Katika wilaya ya Kusini Unguja kuna mji mdogo

unaoitwa Makunduchi, hapa ndipo jina la asili la lahaja hii lilipotoka. Maeneo mengine mnamozungumzwa lahaja ya Kimakunduchi ni Paje, Jambiani, Bwejuu, Pete, Jozani, Mtende, Kizimkazi, Kitongani, Mungoni, Muyuni na Kibuteni. Lahaja hii inajulikana pia kwa jina la Kihadimu na Kikae. Hata hivyo kwa mujibu wa maelezo ya watoa taarifa wengi jina la Kihadimu hivi sasa halitumiki tena kwa kuwa linanasibishwa na utumwa.[1] Hivi sasa majina yanayotumika sana ni Kimakunduchi na Kikae.

Katika maandiko mengi ya zamani, lahaja ya Kimakunduchi iliitwa kwa jina la Kihadimu (taz. k.m. Stigand, 1915; Byran, 1959; Polome, 1967; Whiteley, 1969; Heine, 1970; Dalby, 1977 na Chiraghdin na Mnyampala, 1977).[2] Hata hivyo, baadhi ya waandishi waliotumia jina la Kihadimu walirejelea jamii pana zaidi ya hii inayosemekana sasa kuwa inazungumza Kimakunduchi au Kikae. Kwa mfano, Stigand (1915: 26) anasema kwamba Kihadimu ni lahaja inayozungumzwa katika eneo la Mashariki na Kusini mwa kisiwa cha Unguja. Anaendelea kueleza kwamba, kwa upande wa Kaskazini lahaja hii inajulikana kwa jina la Kitumbatu. Hivyo, kwa mtazamo wa Stigand, Kihadimu na Kitumbatu yanatumiwa kama majina mbadala.

2.1 Asili ya jina la Kihadimu

Kwa kuwa jina la Kihadimu limekuwa likitumiwa na waandishi wengi, itakuwa jambo jema ikiwa tutajadili japo kwa muhtasari kuhusu asili[3] ya jina hili. Katika kulifikia lengo hili, tutajadili kwa muhtasari maelezo ya kihistoria tuliyoyapata kutoka kwa baadhi ya watu tuliowahoji kuhusu asili ya jina hili. Mhojiwa mmoja, anatueleza kisasili[4] kimoja kinachonasibishwa na asili ya jina la Kihadimu. Kisasili chenyewe kilikuwa kama ifuatavyo:

> Miaka mingi iliyopita watu wa Makunduchi na miji ya jirani inayowazunguka walikuwa na maisha yao pamoja na lugha yao[5]. Watu hawa waliishi kwa ushirikiano na upendo wa hali ya juu. Siku moja wakavamiwa na Wareno, ambao walianza kupora mali za wenyeji hawa wa Makunduchi. Hapo ndipo ilipowalazimu kuomba msaada kwa Mwarabu mmoja aliyejulikana kwa jina la

[1] Kamusi ya Kiswahili Sanifu inafafanua maana ya neno *hadimu* kwamba ni mtu anayemtumikia mtu mwingine.

[2] Kwa maelezo zaidi kuhusu kazi za wataalamu hawa tazama Temu (1980:4B).

[3] Neno asili katika muktadha wa makala haya linatumiwa kwa maana ya namna kitu kilivyoanza.

[4] Neno kisasili katika muktadha wa makala haya linatumiwa kwa maana ya mapokeo kutoka kwa wahenga kuhusu asili ya majina mbalimbali.

[5] Baadhi ya watoa taarifa walipoulizwa kuwa lugha hiyo ni ipi walieleza kwamba walisikia kutoka kwa wazee wao kwamba lugha hiyo ni Kimakunduchi.

> Seyyid Hariri. Mwarabu huyu akakubali kuwasaidia. Baada ya kushinda vita ile, Mwarabu akadai ujira wake kwa kazi aliyoifanya. Wananchi wale wakamjibu, "tutawale, sisi ni wahadimu wako". Kuanzia wakati huo jina hili liliota mizizi na kuanza kutumiwa na watu wengi, wakiwemo waandishi wa vitabu mbalimbali.

Ijapokuwa ni vigumu kuthibitisha kama madai yaliyoelezwa hapo juu ni ya kweli au la, lakini angalau tunapata picha kidogo kuhusu asili ya neno hili. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013), inaeleza maana ya neno *hadimu* kwamba ni *mtu anayemtumikia mtu mwingine.* Ukichunguza maana iliyotolewa katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu, utaona kwamba inaendana na maelezo yaliyotolewa katika kisasili hapo juu. Hivyo kisasili hiki kinaweza kuwa na mchango mkubwa katika mjadala wenye lengo la kutaka kujua sababu hasa ya watu wa Makunduchi kuitwa Wahadimu.

Baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, jina hili lilipigwa marufuku kwa madai kwamba linawadhalilisha Wazanzibari na badala yake majina ya Kikae na Kimakunduchi yakaanza kutumika kama mbadala wa jina la Kihadimu.[6] Akijadili zaidi kuhusu majina ya Wahadimu na Wamakunduchi, Iddi (2011:3-4) anasema:

> Licha ya kwamba watu walio nje ya Makunduchi hutumia majina ya Kimakunduchi na Kihadimu kama visawe, ukweli ni kwamba, Wahadimu na Wamakunduchi ni watu tofauti kabisa. Wamakunduchi ni wazawa wa eneo la Makunduchi na ambao hutumia Kimakunduchi katika mawasiliano yao na Wahadimu ni watu waliofika Makunduchi miaka mingi iliyopita kama watumwa na mpaka sasa bado wanaishi humo.

Maelezo ya Iddi yanaibua maswali mengi: Kwa kuwa tumeelezwa kwamba Wamakunduchi na Wahadimu ni watu tofauti; je, lahaja inayorejelewa kama Kimakunduchi hivi sasa, ni ile ya Wamakunduchi wa asili au ni ya Wahadimu ambayo yamkini si Kimakunduchi safi? Kama wenyeji wa Makunduchi na maeneo ya jirani walikuwa wakizungumza Kimakunduchi na hatimaye Wahadimu nao wakawaiga, ni kwa nini waandishi wengi wa zamani hawakutaja jina hili la Kimakunduchi na badala yake wakataja Kihadimu? Je, watumwa hawa walikuwa na umaarufu kiasi gani hadi lugha yao ambayo ni ya tabaka tawaliwa ionekane kuwa na nguvu kiasi cha kuizidi lugha ya wenyeji wao ambayo ni ya tabaka tawala?

[6] Tulipotaka kujua ni nani aliyepiga marufuku matumizi ya jina la Kihadimu, tulielezwa kwamba ni Rais wa awamu ya Kwanza baada ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Maelezo haya pia yanapingana na nadharia za isimujamii kama anavyoeleza Massamba (2002:30) kwamba lugha huweza kubadilika na kuchukua sifa za lugha nyingine hasa katika mazingira ambamo lugha hiyo inaonekana kuwa ni bora zaidi. Ubora unaweza kuwa umetokana na lugha hiyo kuwa lugha ya watu wa tabaka tawala, lugha ya tabaka tajiri, lugha ya watu mashuhuri, lugha ya watu wenye maendeleo makubwa, lugha ya wasomi, n.k. Hivyo, kwa kuwa Wamakunduchi ndio wanaosemekana kwamba ni wazawa wa asili wa Makunduchi, tulitegemea kwamba lugha yao ndiyo ingekuwa maarufu na kurejelewa na waandishi wengi waliotangulia lakini badala yake jina la Kihadimu ndilo ambalo limekuwa likitumika kwa muda mrefu. Tunakubaliana na Iddi kwamba jina la Kihadimu limekuwa likitumiwa zaidi na wageni kwani si ghalibu kwa mtu kutumia jina ambalo yeye mwenyewe anaona kuwa linamdhalilisha.

Hata hivyo, suala la kusikitisha zaidi ni kwamba, Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI, 2004:163) ambayo waandishi wake ni wenyeji wa lugha ya Kiswahili, imefuata mkumbo huohuo wa waandishi wa kigeni, kwa kueleza kwamba, *Kihadimu* ni "lahaja mojawapo ya Kiswahili isemwayo Kusini Mashariki mwa kisiwa cha Unguja". Katika kamusi hiyohiyo, tunaelezwa pia kwamba neno *hadimu* maana yake ni "mtu anayemtumikia mtu mwingine". Katika mazingira kama haya, jina hili halikupaswa kuingizwa katika kamusi hii kuwa ni lahaja mojawapo ya Kiswahili, vinginevyo jina hili lingeweza kuingizwa tu kwa sababu za kihistoria na maelezo yake yangetakiwa kuonesha hivyo.

Katika utafiti tulioufanya eneo la Jambiani wakati wa utafiti wa Mradi wa Lahaja mwaka 2010, tulielezwa kwamba jina *hadimu* lilianza kutumiwa na Waarabu kuwaita wenyeji wa maeneo ya Kaskazini na Kusini mwa kisiwa cha Unguja waliokuwa wakiwatumikia katika shughuli mbalimbali. Hata hivyo, wenyeji wa maeneo haya waliendelea kulitumia jina hili kwa maana ya watu wa asili wa maeneo haya ambao hawajachanganya damu na wageni. Mtazamo kama huu walionao wenyeji wa maeneo haya uliwahi kutolewa pia na Knappert (1992:16) kwa kusema:

> *Jina* hadimu *limetafsiriwa kwa makosa kwa maana ya* mtu anayemtumikia mtu mwingine. *[Anaendelea kueleza kwamba] watu wanaotafsiri jina hili kwa makosa wanalihusisha na neno la Kiarabu* khadim *lenye maana iliyoelezwa hapo juu kwamba* ni mtu anayemtumikia mtu mwingine. *Hata hivyo ukweli ni kwamba jina hili linatokana na neno la Kiarabu* qadimu lenye maana ya kale au asili. *Hivyo [kwa mtazamo wa Knappert] neno* hadimu *linatumika kuwarejelea watu wa asili wa Zanzibar ambao hawakuathiriwa na wageni hasa Waarabu.*
>
> (Tafsiri na mabano mraba ni yangu)

Hivyo, ukiyachunguza maelezo ya Knappert pamoja na yale waliyoyatoa baadhi ya wakazi wa Kusini Unguja utabaini kwamba bado kuna umuhimu mkubwa wa kuendelea kulifanyia utafiti jina la *Kihadimu* ili kuwa na hoja kuntu kuhusu asili ya jina hili.

Ukipitia maandiko mengi yanayohusu lahaja za Kiswahili, utaona kwamba jina la Kimakunduchi limeanza kutumika mwishoni mwa miaka ya 1970. Hata hivyo, kwa sasa Kimakunduchi na Kikae hutumiwa kama majina mbadala. Majina haya yote mawili yanahusishwa na eneo maalumu la kijiografia. Katika wilaya ya Kusini Unguja, kuna eneo linaloitwa Makunduchi na pia kuna eneo linaloitwa Kae Kuu. Maeneo haya yote ni muhimu katika historia ya jamii ya Wamakunduchi. Kae Kuu, kwa mfano, ni mahali ambako shughuli muhimu za kijadi kwa Wamakunduchi hufanyika. Miongoni mwa shughuli hizo ni sherehe za Mwaka Kogwa[7] na mambo mengine ya kijadi, vikiwemo vibanda vya mizimu mbalimbali.

Hivyo, kwa kuwa majina haya "Kimakunduchi" na "Kikae" yanahusishwa na eneo maalumu la kijiografia, inakuwa rahisi kuzoeleka kwani kuna lahaja nyingi za Kiswahili ambazo zimehusishwa na eneo maalumu la kijiografia. Ni katika muktadha kama huu ndipo tunaposikia kwa mfano, watu wakisema lahaja ya Kipemba inazungumzwa katika kisiwa cha Pemba, lahaja ya Kiamu inazungumzwa katika kisiwa cha Lamu na Kitumbatu ni lahaja ya Kiswahili inayozungumzwa katika kisiwa cha Tumbatu.

2.2 Asili ya Jina la Makunduchi

Tumeeleza hapo juu kwamba Kimakunduchi ni lahaja inayozungumzwa katika mji wa Makunduchi na viunga vyake. Hivyo, kimantiki, asili ya jina la Kimakunduchi itapatikana kwa kuchunguza asili ya jina la Makunduchi. Vipo visasili vingi vinavyoeleza asili ya jina la Makunduchi. Mhojiwa mmoja, alipoulizwa kuhusu asili ya jina "Makunduchi" alikuwa na haya ya kusema:

> Inasemekana kwamba kulikuwa na kundi moja la watu waliokuwa wakiishi huko Kae, Pwani; baadhi yao waliondoka kuelekea Kusini Mashariki kupitia sehemu mbalimbali, hatimaye wakafikia sehemu yenye udongo mwekundu.

[7] Hili ni tukio muhimu sana la kijadi kwa Wamakunduchi ambalo hufanyika mara moja kwa mwaka. Kwa maelezo zaidi kuhusu dhana ya Mwaka Kogwa na umuhimu wake, tazama makala ya Mohamed (2010) katika Jarida la *KISWAHILI* Juzuu na.72., uk.108-121.

> Hapa kundi hili lilisita kwanza na kuanza shughuli za kilimo. Baada ya muda fulani wengine walirudi kule Kae, Pwani na walipoulizwa na wenzao walikuwa wapi, wakajibu, "Tuwa uko nyikundu chi" kwa maana kwamba walikuwa wakiishi mahali ambako ardhi yake ni nyekundu. Kwa kuwa hawakuweza kulipata jina hasa la mahali penyewe, hivyo tamko *nyikundu chi* liliwakalia wepesi zaidi. Hivyo, taratibu jina hili likaanza kufanyiwa mabadiliko madogomadogo na hatimaye likapatikana jina la Makunduchi na lugha ya watu hawa ikaitwa Kimakunduchi.

Kwa Kimakunduchi, neno *chi* lina maana ya nchi au ardhi (taz. k.m. Chum, 1994:13). Hivyo maelezo yaliyotolewa hapo juu kuhusu asili ya jina Makunduchi yanaweza kuwa na mantiki.

Hivyo basi, kwa kuwa visasili hivi vimetolewa na watu wengi, na kwa kuwa maelezo yaliyotolewa katika visasili hivyo yana mantiki, tunashawishika kukubalina na mtoa taarifa tuliyemnukuu hapo juu, aliyetueleza kuhusu asili ya jina la Makunduchi na ambaye maelezo yake yaliungwa mkono na watoa taarifa wengine.[8] Maelezo kuhusu visasili hivi yametolewa pia na Juma (2011:29, 34). Hata hivyo mabadiliko ya silabi kutoka "nyi" katika nyikunduchi na kuwa "ma" katika Makunduchi hayana budi kufanyiwa uchunguzi wa kina wa kifonolojia ili kuona uwezekano wa mabadiliko hayo kutokea katika lahaja hii.

2.3 Chimbuko la Wamakunduchi

Baada ya kujadili kwa muhtasari kuhusu usuli na asili ya "Makunduchi", na "Kihadimu", itakuwa vema pia tukapitia mitazamo mbalimbali kuhusu chimbuko[9] la watu wa Makunduchi. Madumulla (1995:45-46) anatueleza kwamba chimbuko la Wamakunduchi halifahamiki vizuri kwani hata jina lenyewe la Wamakunduchi na Kimakunduchi limeanza kuonekana katika maandishi ya hivi karibuni. Katika utafiti tulioufanya katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Kusini Unguja, ilibainika kwamba watoa taarifa walitofautiana kimtazamo kuhusu chimbuko la Wamakunduchi. Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba kuna makundi makuu matatu yanayoelezea kuhusu chimbuko la watu wa Makunduchi.

Kundi la kwanza ni wale wanaodai kwamba watu wa mwanzo kuishi Makunduchi walitoka Tumbatu na kufikia eneo liitwalo Nganani ambalo liko

---

[8] Tunatambua kwamba, kuna visasili vingine vinavyoelezea kuhusu asili ya jina la Makunduchi. Miongoni mwa visasili hivyo ni kile cha utani kati watu wa Mtende na Makunduchi. Hata hivyo, kisasili tulichokieleza hapo juu kinaonekana kuwa na mantiki zaidi.

[9] Katika utafiti huu, tunapozungumzia chimbuko la watu fulani, tuna maana ya mahali ambako watu hao walitokea.

Kaskazini-Mashariki mwa Makunduchi. Watoa taarifa hawa wanaendelea kueleza kwamba, ndiyo maana hadi sasa lahaja za Kimakunduchi na Kitumbatu zinafanana kwa kiasi kikubwa hata zikawafanya watu kama Stigand (1915) wakaona kwamba Kimakunduchi (ambacho yeye alikiita Kihadimu) na Kitumbatu ni majina mbadala.

Watoa taarifa hawa walipoulizwa kuhusu watu waliokuweko eneo la Nganani kabla ya ujio wa watu kutoka Tumbatu, walikuwa na mitazamo inayopishana; kuna waliodai kwamba mahali hapo na eneo lote la Makunduchi hapakuwa na watu, bali waliishi majini, na wengine wakaeleza kwamba, eneo hilo lilikuwa na watu japo haifahamiki bayana kwamba watu hao ni akina nani na walitoka wapi. Maelezo ya jumla tuliyoyapata kutoka kwa watu wa kundi hili yanatupa picha kuhusu uhusiano uliopo baina ya Wamakunduchi na Watumbatu, kwamba kuna uwezekano watu hawa wakawa na uhusiano wa kimnasaba.

Kundi la pili linawahusisha watoa taarifa wanaojinasibisha na Ushirazi. Watu hawa wanaeleza kwamba Washirazi kutoka Iran walifika Kusini mwa Unguja hasa maeneo ya Bwejuu wakitokea maeneo ya Kaskazini hasa Tumbatu. Juma (2011:35) amenukuu maelezo ya *Bwana Bindu*[10] akielezea kuhusu asili ya watu wa Bwejuu kama ifuatavyo:

> Asili ya Wabwejuu ni Washirazi kutoka Pashia huko Iran. Watu hawa walifika Bwejuu wakitokea Kaskazini, maeneo ya Nungwi na Tumbatu. Inasemekana kwamba Tumbatu ambayo iko Kaskazini mwa Unguja ndiyo sehemu ya mwanzo kabisa kukaliwa na watu wa Unguja. Watu hao walipitia sehemu mbalimbali kabla ya kuingia Bwejuu. Walipitia Ntaiwe, ambayo ni Charawe ya sasa. Pia waliishi Unguja Ukuu, ambao ni mji wa mwanzo kabisa kwa upande wa Kusini kuanza kuishi watu. Baada ya kutokea njaa kali walihama huko na kuelekea Kiungani, maili tano kutoka Bwejuu ambako walikuta mchanga mweupe, gofu la msikiti na visima vitatu. Hii ilikuwa karne ya 12. Waliona bora waishi katika mazingira yenye maji baada ya kukosa pepo za msimu ambazo zingesaidia usafiri wao kwa njia ya bahari kwa kutumia majahazi. Hawa walikuwa ni wafanyabiashara. Watu hao wenye asili ya Kiajemi waliwakuta watu tayari wanaishi Unguja Ukuu, Kidoti na Fukuchani.

Maelezo haya yanafanana na yale ya kundi la kwanza lililodai kuwa asili ya watu wa Makunduchi ni Tumbatu. Hoja kwamba Tumbatu ndiyo sehemu ya mwanzo kabisa kukaliwa na watu Unguja, na kwamba watu wa mwanzo kufika Bwejuu (ambayo ni miongoni mwa maeneo ambako lahaja ya Kimakunduchi

[10] Huyu alikuwa ni miongoni mwa watoa taarifa kutoka Bwejuu.

inazungumzwa) walitoka Tumbatu, inaendana na madai yaliyotolewa hapo juu kwamba hapo zamani za kale kuna kundi moja la watu waliotoka Kaskazini mwa Unguja na kufikia eneo liitwalo Nganani ambalo liko Kaskazini-Mashariki mwa Makunduchi.

Hata hivyo, maelezo yaliyotolewa hapo juu, kwamba watu hawa walipofika Kiungani walikuta gofu la msikiti na visima vitatu, ni ishara kwamba, eneo hili lilishakaliwa na watu kwa muda mrefu, tena yumkini watu hawa walikuwa ni wageni. Hoja hii ya kuona kwamba yawezekana watu waliokuwa wakiishi Nganani walikuwa wageni, inatokana na gofu la msikiti walilolikuta wahamiaji hawa kutoka Tumbatu. Hali hii ni kutokana na kuwa imani ya dini ya Kiislamu na ujenzi wa msikiti vililetwa Pwani ya Afrika Mashariki na wageni, hasa Waarabu kutoka Mashariki ya kati. Hata hivyo kwa mujibu wa utafiti tulioufanya Zanzibar, tumebaini kwamba misikiti ya mwanzo kujengwa katika maeneo mbalimbali ya kisiwa hiki, ilijengwa na Washirazi kutoka Iran na wala sio Waarabu kama watu wengi wanavyoamini. Ni kutokana na hoja hii ndipo tunakuta kwamba watu wengi wa maeneo haya wanajinasibisha sana na Ushirazi.

Mfano mmojawapo ni msikiti wa Kizimkazi, unaosemekana kwamba ulijengwa na wageni kutoka Iran mwanzoni mwa karne ya 12 (mwaka 1107). Hata maandishi yaliyoandikwa ndani ya msikiti si ya Kiarabu, bali inasemekana kuwa ni maandishi ya Kiajemi. Tulipofanya utafiti eneo la Kizimkazi mtoa taarifa mmoja alitueleza kwamba, miaka ya hivi karibuni waliwahi kuja watu kutoka Iran wakidai kuwa ule msikiti ulijengwa na babu zao. Maelezo yanayotolewa na mtoa taarifa huyu ni ithibati kwamba watu waliohusika na ujenzi wa msikiti wa Kizimkazi walitoka Iran. Watu wa Iran kwa asili yao si Waarabu bali ni Waajemi. Hivyo, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kwamba wageni wa mwanzo kufika maeneo ya Kusini Unguja na kujenga misikiti walikuwa ni Waajemi kutoka Iran.

Suala la kuwahusisha Washirazi na maendeleo ya awali katika miji ya Waswahili haliwahusu watu wa Makunduchi peke yake, bali pia maendeleo ya miji mingine ya Pwani yamehusishwa sana na ujio wa Washirazi. Kwa mfano, Hollingsworth (1929:39), anaelezea kuhusu waanzilishi wa mji wa Kilwa, kwa kusema:

> Tumekwishajifunza kwamba waanzilishi wa mji wa Kilwa ni Washirazi. Ustaarabu ulioinukia katika karne ya 10, 11 na 12 [hasa katika ujenzi wa misikiti] ulikuwa ni wa Kishirazi au Kiajemi. Hadi hivi sasa sehemu kubwa ya watu wa upwa huu [Pwani ya Afrika Mashariki] wananasibisha sana asili yao na Ushirazi au Uajemi (Tafsiri na msisitizo wa mabano - mraba ni yangu).

Tunayaafiki maoni ya Hollingsworth kwamba Washirazi wamehusishwa sana na ujenzi wa misikiti mingi ya kale (kama ile ya Kizimkazi, Tumbatu na Kilwa). Tunaafikiana naye pia kwamba baadhi ya wakazi wa mwambao wa Afrika Mashariki (wakiwemo watu wa Makunduchi) wanapenda kujinasibisha na Ushirazi kuliko Uafrika. Hata hivyo, tunachelea kukubaliana naye kwamba Washirazi ndio waanzilishi wa miji ya Pwani ukiwemo mji wa Kilwa na kuwa ustaarabu wa maeneo haya uliletwa na Washirazi. Kukubaliana na maelezo yake kuna maana kwamba kabla ya ujio wa Washirazi miji hii haikuwa na wakazi wake wa asili, jambo ambalo halina ushahidi usiosailika.

Kuna waandishi wengine wanaeleza kwamba uhusiano baina ya watu wa Afrika Mashariki na wenzao wa Ghuba ya Uajemi ulianza siku nyingi hata kabla ya karne ya juhudi za kueneza Uislamu kuanza. Kwa mfano, Gray (1955:6) anaeleza:

> Kuna ushahidi wa kutosha unaoonesha kwamba miaka mingi iliyopita kulikuwa na mwingiliano wa karibu baina ya wakazi wa Afrika Mashariki na wenzao kutoka Ghuba ya Uajemi. Mathalani kati ya mwaka 293 na 302 BK inasemekana kwamba Zand Afrik Sha (haya ni maneno ya Kiajemi yenye maana ya mtawala wa sehemu ya upwa wa Afrika Mashariki) alituma salamu za pongezi kwa mtawala mpya wa Kiajemi aliyeitwa Narsen.
>
> (Tafsiri na msisitizo wa mabano ni wangu).

Maelezo haya yanaashiria kwamba kulikuwa na uhusiano wa karibu kati ya wakazi wa Afrika Mashariki na watu wa Ghuba ya Uajemi kuanzia karne ya tatu.

Pamoja na maelezo marefu kuhusu ujio wa wageni katika wilaya ya Kusini Unguja, bado hakuna ushahidi usiosailika unaoweza kutudhihirishia kwamba wageni kutoka Iran walipofika katika maeneo ya upwa wa Afrika Mashariki hapakuwa na wenyeji waliokuwa wakiishi katika maeneo haya. Hivyo ni vigumu kukubaliana na wazo kwamba chimbuko la watu wa Makunduchi ni Shirazi, japo tunakiri kwamba maelezo kuhusu ujio wa Washirazi yametusaidia sana katika kupata picha kuhusu ujio wa wageni katika upwa wa Afrika Mashariki.[11]

Kundi la tatu ni watoa taarifa wanaodai kwamba watu wa mwanzo kufika Makunduchi walitoka Tanzania bara. Waumini wa kundi hili ni wengi ila

[11] Licha ya baadhi ya watu kujinasibisha na wageni, hasa wa kutoka Mashariki ya kati, hakuna mtoa taarifa hata mmoja aliyedai kuwa asili yake ni Arabuni. Hali hii inaashiria kwamba huenda majumuisho mengi yanayofanywa kuhusu ujio wa Waarabu kama wageni wa mwanzo kufika upwa wa Afrika Mashariki na kujenga misikiti pamoja na kueneza dini ya Kiislamu, hufanywa kwa ujumla sana.

wanatofautiana kuhusu mahali hasa walipotoka watu hawa kwa upande wa Tanzania bara. Baadhi ya maeneo yanayotajwa kuwa ndiko walikotoka Wamakunduchi ni pamoja na Kunduchi na Kimbiji (Dar es Salaam), Kaole na Mlingotini (Bagamoyo), Mafia, Songosongo na Somanga (Kilwa).

Ukiyachunguza vizuri maeneo haya yote yanayotajwa kuwa ndiko walikotoka Wamakunduchi, utabaini kwamba maeneo mengi kama siyo yote, yako ukanda wa pwani. Hivyo kwa maelezo haya, ni ishara kwamba lugha za Pwani zina mchango mkubwa katika kupata asili ya Wamakunduchi. Kutokana na maoni haya yanayohusisha chimbuko la Wamakunduchi na watu wa bara ndiyo maana baadhi ya watu wanaamini kwamba lahaja ya Kimakunduchi, inafanana sana na lugha za bara (hasa zile za pwani) kuliko inavyofanana na lahaja nyingine za Kiswahili zilizoko katika kisiwa cha Zanzibar. Akishadidia hoja hii, Idris Abdul Wakil[12], aliyeandika dibaji ya *Kamusi ya Msamiati Pekee wa Kikae* (1994), alikuwa na haya ya kusema:

> Kikae ni Kiswahili ambacho husemwa huko Makunduchi, yaani Kae. Lakini ndani yake yamo maneno mengi sana ambayo hayana asili ya Kiswahili. Inawezekana maneno hayo yameazimwa kutoka katika lugha kadhaa zisemwazo Tanzania bara, Kenya na kwingineko. Vilevile ni shida sana kwa mtu ambaye hakuzaliwa na hasa kukulia Makunduchi kuweza kukisema kwa fasaha nzuri. Watu wengi hujaribu kukisema lakini mara hushindwa katika matamshi. Kwa sababu hiyo baadhi ya watu hufikiri kuwa Kikae ni lugha tofauti na Kiswahili.

Maelezo ya Abdul Wakil ya kukinasibisha Kimakunduchi na lugha nyingine za bara, ni ithibati kwamba yawezekana wazungumzaji wa lahaja hii chimbuko lao ni Tanzania bara.

Ukizifuatilia kwa makini hoja za makundi yote matatu kuhusu chimbuko la Wamakunduchi, utakubaliana nasi kwamba hoja za kundi la tatu zina ushawishi mkubwa zaidi kutokana na sababu kuu mbili. Sababu ya kwanza ni kwamba, baadhi ya majina ya maeneo yanayotajwa kwamba ndiko walikotoka Wamakunduchi wa mwanzo, yanapatikana pia katika maeneo mnamozungumzwa lahaja ya Kimakunduchi. Eneo mojawapo ni Kaole (Bagamoyo). Katika mji wa Makunduchi kuna eneo pia linaitwa Kaole. Jina la Makunduchi pia kwa kiasi fulani linanasibishwa na Kunduchi iliyoko Dar es Salaam kunakosemekana kwamba ni asili ya watu wa Makunduchi. Sababu ya pili ni kuhusu msamiati kama alivyosema Abduli Wakil, kwamba lahaja hii ina maneno mengi ambayo kwa mtu ambaye hajakulia Makunduchi hushindwa hasa katika matamshi.

[12] Huyu alikuwa rais wa nne wa Zanzibar.

Msamiati huu unahusishwa zaidi na lugha zilizoko Tanzania bara na kwingineko (hasa zile zilizoko maeneo ya Pwani).

3.0 Hitimisho

Maelezo tuliyoyatoa hapo juu mbali na kueleza kuhusu chimbuko la watu wa Makunduchi yanatupa picha pia kuhusu ujio wa wageni mbalimbali katika upwa wa Afrika Mashariki. Ingawa taarifa tuliyonayo kwa muda mrefu inadai kwamba watu wa mwanzo kufika Pwani ya Afrika Mashariki na kujenga misikiti pamoja na kueneza dini ya Uislamu ni Waarabu. Hata hivyo, maelezo tuliyoyapata kutoka kwa watoa taarifa kutoka Makunduchi, na kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali vya kihistoria tulivyovijadili, mwelekeo ni tofauti kwani ujenzi wa misikiti ya mwanzo kujengwa maeneo mbalimbali kama Kizimkazi, Tumbatu na Kilwa, inasemekana kwamba ilijengwa na Washirazi kutoka Ajemi.

Marejeo

Chiraghdin, N. & M. Mnyampala (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Gray, J. M. (1955). "Nairuzi or Siku ya Mwaka" katika *Tanganyika Notes and Records*. 38:1-22.

Gray, J. M. (1977). "The Hadimu and Tumbatu of Zanzibar" katika *Tanganyika Notes and Records* 81/82:135-153.

Harries, L. (1964). "The Arabs and the Swahili Culture" katika *Africa*, Juzuu xxxiv/3: 224-230.

Iddi, Z. A. (2011). *Phonological Processes in Kimakunduchi*, Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Juma, H (2011). *Tofauti za Kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili cha Wete katika kisiwa cha Pemba* Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Madumula, J.S. (1995). "Mwaka-Kogwa [au nairuz] katika Makunduchi" katika Mlacha S.A. K & Hurskainen, A (wah.) *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massamba, D.P.B. (1989b). "An Assessment of the Development and Modernization of the Kiswahili language in Tanzania" katika Coulmas, F (mh.), *Language Adaptation*, Cambridge: Cambridge University Press, uk.60-78.

_____ (2002). *Historia ya Kiswahili: 50 BK hadi 1500 BK*. Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Mohamed, M (2010). "Mwaka Kogwa na Changamoto Zake" katika D. P. B Massamba (mh.) *Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, M. M. (2005). "Miaka 75 ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1930-2005)", katika J.S Madumla na Y.M Kihore, (wah.) *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mwansoko, H. na Z. Masabo (1992). *Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Nurse, D. na T. Spear (1985). *The Swahili: Reconstructing The History and Language of an African Society, 800-1500*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook*, Washington DC: Centre for Applied Linguistics.

Rolleston, I. H.O. (1939). "The Watumbatu of Zanzibar" katika *Tanganyika Notes and Records 8: 85-97.*

Stigand, C. H. (1915). *A Grammar of Dialectical Changes in the Kiswahili Language*, Cambridge: Cambridge Universiry Press.

Temu, C.W. (1980). *Lahaja za Kiswahili: Muswada wa Ripoti ya Mwanzo ya Mradi wa Lahaja*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Pili), Nairobi: Oxford University Press.

Whiteley, W. (1958). *Dialects and Verse of Pemba: An Introduction*. Kampala: East African Swahili Committee

Whiteley, W. (1969). *Swahili: The Rise of a National Language*, London: Methuen & Co. Ltd.